



Jarida Mtandao

TACAIDS



TACAIDS YAWEKA MIKAKATI MADHUBUTI KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI



ya teknolojia katika utoaji wa huduma, kuongezanguvu kufikia vijana hasa walioko vijijini, elimu zaidi katika maeneo ya starehe ikiwemo kumbi za miziki na makongamano ya vijana lengo ni kuhakikisha jamii inafikiwa kwa ukubwa wake.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Mhe. Dkt. Johannes Lumbulung Lukumay ameipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna inavyoratibu masuala ya Afua za UKIMWI nchini huku akieleza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha Utekelezaji wa Afua hizo unafanikiwa bila mkwamo wowote.

Pia wajumbe wa kamati hiyo wamepongeza na kuishukuru Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa Dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARVs) zinazosaidia kuimarisha kinga ya mwili, kuzuika VVU kujizalisha mwilini na kushusha kiwango cha Virusi hadi kutokuonekana ili kuzuia maambukizi mapya kwa jamii.

Akifafanua hoja za wajumbe wa kamati hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Adam Mrisho amesema, ofisi yake imeendelea kuweka mikakati madhubuti na hatua za makusudi katika kuhakikisha utekelezaji wa Afua za UKIMWI unafanyuka vyema na kuyafikia makundi yote hususan vijana.

Dodoma, 20, August 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) inaendelea kuimarisha mikakati madhubuti ya kupambana na VVU na UKIMWI kupitia ushirikiano wa kisékta, kuhamasisha vyanzo vya fedha vya ndani, kusogeza huduma karibu na jamii ikiwemo Vituo vya Maarifa kwa madereva wa malori na kuwajengea uwezo vijana na wanawake ili kufikia lengo la kutokomeza kabisa janga hili ifikapo mwaka 2030.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilipokutana kwa lengo la kupokea taarifa ya wasilisho la hali ya Maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa Vijana na Mikakati wa Kupunguza Maambukizi Mapya kwa Vijana, kilichofanyika tarehe 20 Agosti, 2026 Bungeni Jijini Dodoma.

Waziri Kabudi ameipongeza Kamati kwa namna ilivyoshauri na kupendekeza uboreshwaji wa masuala mbalimbali ikiwemo matumizi

“Ni vyema sasa kuendelea kuwajengea uwezo vijana katika mikoa yenye ushamiri mkubwa wa maambukizi na kuratibu utoaji wa elimu na upimaji wa hiari katika maeneo ya kazi na sekta ya usafirishaji hususan kwa madereva wa malori wa masafa marefu,” alisema Dkt. Lukumay Vilevile ameipongeza Serikali kwa namna ilivyowekeza nguvu kuhakikisha janga hili linatokomezwa pamoja na kubuni program na miradi mbalimbali ikiwemo ya TIMIZA Malengo Awamu ya Tatu, inayoendeshwa na kauli mbiu isemayo; “Tusonge na Samia kutokomeza UKIMWI, ambavyo vinaleta mwamko wa jamii kujitokeza kupima afya zao na kuendelea kuchukua tahadhari juu ya maambukizi mapya ya VVU.

“Tume imejipanga kuhakikisha elimu inaendelea kuifikia jamii ili kuwa na utayari wa kupima na kuhamasisha matumizi ya dawa kwa watakapo gundulika kuwa na maambukizi ya VVU pamoja na kuimarisha mashirikiano na sekta binafsi” alieleza Dkt. Mrisho Jitihada zingine ni kuwezesha wahudumu ngazi ya jamii wapatao elfu tisini kwa kuwapatia elimu ya kutoa huduma za kinga na huduma za JIPIE, hivyo kusaidia kuwafikia vijana waliopo vijijini na kuongeza mwingi wa masuala ya UKIMWI.

Pia mikakati mingine ni kuviwezesha na kuboresha vituo 32 vya maarifa vinavyotoa elimu ya kinga, huduma za ARVs, upimaji na kuhakikisha vijana wanapewa elimu za masuala ya UKIMWI hususani madereva wa malori ya masafa marefu kupitia vituo hivyo vilivyopo nchini.



NAIBU WAZIRI UMMY NDERIANANGA ATEMBELEA BANDA LA TACAIDS KATIKA MAONESHU YA NANENANE – DODOMA

Agosti 6, 2026

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Mhe. Ummy Nderiananga, ametembelea banda la Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS lililopo katika Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, kwenye Viwanja vya Maonesho ya Nanenane vya Dkt. John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma.

Akiwa katika banda hilo, Mhe. Nderiananga amepata



elimu kuhusu VVU kushirikiana na na UKIMWI pamoja Serikali na wadau na taarifa kuhusu hali mbalimbali katika maambukizi nchini kuendelea kuimarisha mwitikio wa VVU na hatua mbalimbali zina zochukuliwa na UKIMWI kupitia Serikali katika utoaji wa elimu, kuimarisha mwitikio wa uratibu wa afua na taifa dhidi ya UKIMWI. huduma zinazolenga kupunguza maambukizi mapya Mhe. Nderiananga amepongeza juhudi na kuboresha maisha zinazofanywa na ya watu wanaoishi na TACAIDS kwa VVU.



SERIKALI KUONGEZA NGUVU MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

Na. Mwandishi Wetu - Shinyanga

SERIKALI imesema itaendelea kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU), kwa kuboresha vituo vya huduma, kuwezesha vikundi na kuimarisha ushirikiano na wadau, ili kuhakikisha Tanzania inafikia lengo la kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Dk. Jim Yonazi, wakati wa ziara yake mkoani Shinyanga, ambapo alitembelea vikundi mbalimbali vya vijana vinaoishi na Maambukizi ya VVU pamoja na Kituo cha Maarifa Kahama kilichopo Kagongwa mkoani humo.

Dk. Yonazi amesema juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau zimeanza kuzaa matunda, huku akisisitiza umuhimu wa kuongeza kasi katika utoaji wa elimu, upimaji, ushauri nasaha, pamoja na huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU.

“Lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma karibu nao, lakini vilevile wanapata elimu inayowasaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI na maambukizi ya UKIMWI,” amesema.

Amesema Serikali imeendelea kuboresha huduma hizo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa wakati, huku akiwataka wadau kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha afua za kukabiliana na VVU.

Dkt. Yonazi amepongeza Mkoa wa Shinyanga kwa kufikia malengo ya kimataifa ya 95-95-95, akisema hatua hiyo ni ishara ya mafanikio katika jitihada za kupunguza

maambukizi mapya na madhara yatokanayo na VVU.

“Serikali imeamua kwa makusudi kabisa kuongeza nguvu yake. Ndiyo maana imeanzisha Mfuko wa Mfadhili, na asilimia 70 ya fedha hiyo inakwenda katika Mfuko wa UKIMWI ili kusaidia afua mbalimbali na kuondokana na utegemezi,” amesema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Mbona Mahita, alisema mkoa huo bado una kiwango cha maambukizi ya VVU kilicho juu ya wastani wa kitaifa, ambapo Shinyanga ina asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ya kitaifa.

Mahita alisema Serikali imeendelea kuongeza elimu kuhusu VVU katika ngazi mbalimbali, kuanzia kaya hadi jamii, ili wananchi wawe na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi.

“Shinyanga ni business hub kwa Kanda ya Ziwa. Movement za watu mara kwa mara ni kubwa. Watu wanaoingia na kutoka ni wengi, ndiyo maana tumeshuka mpaka kwenye ngazi za kijamii katika utoaji wa elimu,” alisema.

Awali, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Honoratha Rutatinisibwa, alisema mkoa huo una vituo 374 vinavyotoa huduma za afya, ambapo vituo 120, sawa na asilimia 32, vinatoa huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU.

Dkt. Rutatinisibwa amesema, kwa mujibu wa utafiti wa maambukizi ya VVU uliofanyika mwaka 2023, kiwango cha maambukizi mkoani Shinyanga ni asilimia 5.6, ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 4.4.

Akizungumzia huduma zinazotolewa katika Kituo cha Maarifa Kahama kilichopo Kagongwa, Mratibu wa Kudhibiti Maambukizi ya VVU, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono Kahama, Dkt. Herry Silvester, amesema kituo hicho kinatoa huduma za tiba na matunzo, pamoja na huduma maalumu kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

Amesema makundi hayo ni pamoja na madereva wa masafa marefu, mabinti na wanawake vijana, ambao wamekuwa wakifikwa kupitia huduma za upimaji, elimu na ushauri nasaha.



MKURUGENZI MTENDAJI TACAIDS ATOA PONGEZI KWA UHAMASISHAJI ULIOFANYWA NA PAZA SAUTI.



Mwanza-Septemba 05, 2026

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS Dkt Adam Mrisho ametoa pongezi kwa vijana wa Vikundi vya Paza Sauti na Dreams kwa ushiriki na juhudi za uhamasishaji walizofanya katika Maonesho ya Biashara ya 21 ya Afrika Mashariki yanayoendelea kwenye Viwanja vya Furahisha, Jijini Mwanza.

Aidha Dkt. Mrisho amesisitiza ubunifu

na ushirikiano kwa vikundi hivyo ili waweze kuongeza uzalishaji na kujitengezea kipato zaidi.

TACAIDS inawakaribisha wananchi wote kutembelea banda letu katika banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu -Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu ili kupata elimu sahihi ya VVU na UKIMWI.





MAONESHU YA WAKULIMA NANENANE – DODOMA

Agosti 8, 2026.
Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS inawakaribisha wana-nchi wote katika Ma-onesho ya Wakulima

Nanenane, kwenye banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kupata huduma za VVU na UKIMWI. Tunatoa huduma za elimu ya VVU na

UKIMWI, upima-ji binafsi wa VVU na ushauri nasaha, pamoja na elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza bila malipo Karibuni sana.

MAONESHU YA BIASHARA YA AFRIKA MASHARIKI

Mwanza- Septemba 01,
2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS inaendelea na uhamasishaji na utoaji wa elimu kuhusu VVU na UKIMWI katika Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayofanyika katika Viwanja vya Furahisha, Jijini Mwanza.

TACAIDS imewapa fursa vijana kutoka vikundi vya Paza Sauti na DREAMS kushiriki katika utoaji wa elimu kuhusu VVU na UKIMWI, kuonyesha na kuuza bidhaa mbalimbali wanaozalisha, ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha vijana kiuchumi.

TACAIDS inawakaribisha wananchi wa Mwanza kutembelea Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, kujipatia elimu sahihi kuhusu VVU na UKIMWI, pamoja na kujionea ubunifu na bidhaa zinazotengenezwa na vijana wa vikundi hivo



MTENDAJI MKUU NACOPHA, AJIONEA UJASIRIAMALI WA PAZA SAUTI

Afisa Mtendaji Mkuu wa NACOPHA Bw. Deogratus Rutatwa ametembelea banda la TACAIDS kwenye banda jumuishi la ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu katika Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayofanyika Viwanja vya Furahisha, Jijini Mwanza na kupatiwa Elimu ya VVU na UKIMWI na kujionea Vijana wa vikundi



vya Paza Sauti na Dreams walivyoweza kutumia elimu ya ujasiriamali waliyopewa chini ya uratibu wa TACAIDS kujitengenezea fursa ya kipato ili kujikwamua kiuchumi

KILI CHALLENGE 2026

Julai 29, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS kwa kushirikiana na wadau wa Geita Gold Mining Limited (GGML) wameshiriki kikao cha pamoja na Wajumbe wa kamati ya maandalizi ya kuwapokea wapanda mlima Kwa miguu na waendesha baiskeli wa Kili challenge 2026 katika ukumbi mdogo wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kikao hicho kimeleenga kujadili mrejesho wa kamati zilizopewa majukumu yakahakikisha maandalizi yanakamilika kuelekea kwenye hafla maalumu ya kuwapokea wapanda mlima kwa miguu na waendesha baiskeli itayofanyika Julai 30, 2026.



DKT. YONAZI AVIASA VIKUNDI VYA WAVIU KUTUMIA MITANDAO YA KIJAMII KUWAFIKIA WATEJA



Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Adam Mrisho alisisitiza kuwa TACAIDS itaendelea kuwekeza katika uwezeshaji wa vijana kiuchumi kama sehemu ya juhudi za kuwaondoa katika mazingira ya changamoto na vishawishi vinavyoweza kuongeza hatari ya maambukizi mapya ya VVU.

“hongereni kwa juhudi na kazi mnazozifanya, hili ni eneo ambalo Tume tumezingatia sana ili kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi” alisema

Na. Mwandishi Wetu - Mwanza

Agosti 17, 2026

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Dkt. Jim Yonazi ashauri kikundi cha Paza Sauti cha Watu Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (WAVIU) kikundi cha Paza Sauti kutumia mitandao ya kijamii kutangaza na la machoni nendeni kuuza bidhaa zao ili duniani kupitia kuweza kufikia wateja mitandao ya kijamii, wengi zaidi huku anzisheni akaunti ya akiwapongeza kwa Instagram muweze juhudi na umoja wao kuwafikia hata watu katika shughuli zao za walipo nchi za nje” alisema Dkt. Yonazi

Ametoa ushauri huo alipotembelea kikundi cha Paza Sauti cha wajasiliamali wanaoishi na VVU katika ziara yake ya ufutilaji utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI katika Wilaya ya Nyamagana, Jijini Mwanza.

Vilevile, Dkt. Yonazi alitembelea Kikundi cha Peace and Love kinachojishughulisha na kilimo cha nyanya na matikiti, kinachosimamiwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kupitia Mradi wa DREAMS, unaoratibiwa na TACAIDS kwa kushirikiana na ICAP, Mradi huo unalenga kuwawezesha wanawake na vijana balehe kiuchumi na kijamii ili kupunguza vishawishi vinavyoweza kupelekea maambukizi mapya kwa kundi hili.

Kwa hatua nyingine Dkt. Yonazi amepongeza Jiji la Mwanza kwa kuweza kufanikiwa kufikia lengo la kitaifa la 95-95-95 kwa kiwango cha juu na kuongeza ushirikiano na wadau wakiwemo viongozi wa dini katika mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini.

Nae, Katibu wa Baraza la Watu Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Wilaya ya Nyamagana Bw. Joseph Kiharate ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu kwa kuwezesha WAVIU kupata dawa katika hospitali zote na kushukuru huduma zinatolewa kwani zinazingatia ubora na weledi kwa kila siku katika juma.

“tunashukuru tunapata dawa katika hospitali zote na huduma zinatolewa siku saba za wiki kupitia nyie afya zetu zinaimarika,” alisema Joseph.



Watumishi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Tanzania - TACAIDS, wakiongozwa na Meneja wa Kanda ya Kati Bw. Yericko Kawanga, kwa kushirikiana na watumishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halmashauri ya Kilolo pamoja na wadau kutoka Afya Yangu na FHI 360/EPIC, wametembelea kituo cha maegesho ya magari ya masafa marefu Ruaha Mbuyuni, mkoani Iringa na kuona shughuli za VVU na UKIMWI zinavyotekelezwa katika eneo hilo.

Katika ziara hiyo, wamepata fursa ya kuzungumza na watoa huduma wa eneo hilo ili kujionea utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI katika eneo hilo, pamoja na kufahamu mafanikio, changamoto na mwitikio wa jamii katika matumizi ya huduma zinazotolewa.

Watoa huduma wameeleza kuwa maambukizi mapya ya VVU katika eneo hilo yameendelea kupungua kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Aidha, wamebainisha kuwa mwitikio wa madereva wa magari ya masafa marefu na wananchi wanaofika katika eneo hilo ni mzuri, huku wengi wakijitokeza kwa hiari kupata huduma za upimaji VVU (PrEP) pamoja na kondomu.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Meneja wa Kanda ya Kati wa TACAIDS Bw. Yericko Kawanga, aliwapongeza watoa huduma na wadau kwa

kujituma katika kuhakikisha huduma za kinga dhidi ya VVU zinawafikia wananchi na kisisitiza kuwa


ushirikiano huo unaendelea kuimarisha Mwitikio wa

kitaifa wa kudhibiti VVU na UKIMWI na kuchangia

kupunguza maambukizi mapya nchini.



HIV



TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA

S.L.P 2904 Nanenane, Nzunguni DODOMA

Barua pepe: info@tacaids.go.tz

Tovuti: www.tacaids.go.tz

tacaidsinfo  www.tacaids.go.tz